NIPASHE: UK9.

# *Mil. 100/- kuweka miundombinu kituo cha vifaranga vya samaki

Na Mbaraka Kambona, RUVUMA

KATIBU Mkuu, Wizara ya Mifugo na Uvuvi (Uvuvi), Dk. Rashid Tamatamah, amesema Serikali imepanga kutumia Sh. milioni 110 kwa ajili ya kuimarisha miundombinu ya Kituo cha Kutotolesha vifaranga vya samaki cha Ruhila ili kiweze kuzalisha vifaranga vitakavyokidhi mahitaji yaliyopo sasa.

Dk. Tamatamah aliyasema hayo alipotembelea kukagua shughuli zinazofanywa na kituo hicho kilichopo mkoani Ruvuma, juzi.

Alisema kwa mwaka huu wa fedha 2020/2021 Serikali imepanga kuzalisha vifaranga milioni 22, na kati ya hivyo, vifaranga mlioni 16 vitazalishwa na vituo vya kutotolesha vya watu binafsi na vifaranga milioni 6 vitazalishwa na vituo vya Serikali.

Dk. Tamatamah aliongeza kuwa hivi karibuni Wizara itatangaza zabuni kwa ajili ya kuimarisha na kuboresha kituo hicho ili kiweze kuwa na uwezo mkubwa zaidi wa kuzalisha vifaranga utakaowezesha kukidhi mahitaji yaliyopo sasa.

"Baada ya kukiimarisha kituo hiki mwaka huu, mwaka ujao wa fedha tutafanya ukarabati mkubwa na ukarabati huo ukikamilika tunatarajia uwezo wa uzalishaji wa kituo hiki kuongezeka mara tatu zaidi ya sasa na hivyo kutaongeza uhakika wa upatikanaji wa vifaranga vya samaki," alisema Dk. Tamatamah

Naye, Mkurugenzi wa Idara ya Viumbe Maji kutoka Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Dk. Nazael Madalla, alitoa rai kwa Watanzania hasa wale wanaoishi mbali na vyanzo vikubwa vya maji kama maziwa kujihusisha na shughuli za ufugaji wa samaki kwani kwa kufanya hivyo kutawasaidia kupata kipato na lishe bora.

Kaimu Katibu Tawala anayeshughulikia Uchumi na Uzalishaji, Mkoani Ruvuma, Deogratius Sibula, alisema Ruhila kimekuwa kituo muhimu sana kwa mikoa ya Nyanda za Juu Kusini kwa sababu wafugaji wengi wanategemea kituo hicho kupata vifaranga vya samaki kwa ajili ya kufuga.

"Katika Mkoa wa Ruvuma kuna Wafugaji wa Samaki takriban 4,000 na kuna mabwawa ya samaki zaidi ya 6,000 na wote wamekuwa wakitegemea kituo hiki kwa ajili ya kupata mbegu na kupata elimu ya ugani, hivyo ni kituo muhimu sana katika kuchagiza ongezeko la ufugaji wa samaki na upatikanaji wa lishe bora kwa Wananchi," alisema Sibula

Scanned with CamScanner

HABARI LEO UK 6.



Na Oscar Job

# Hongereni Arusha utoaji maziwa kwa wanafunzi

SERIKALI kupitia Bodi ya Maziwa Tanzania (TDB) imeanzisha mpango wa kuwapatia maziwa wanafunzi wa shule za msingi nchi nzima ikiinza na mkoa wa Arusha na baadae kwenda nchi nzima.

Lengo la hatua hiyo ni kuwajenga kiafya na kiakili wanafunzi hao sambamba na kuwaongezea uelewa darasani

Mpango huo unaohusisha uchangiaji wa gharama kidogo kutoka kwa mzazi kwa ajili ya kuwezesha upatikanaji wa maziwa hayo kutoka viwandani kuwa endelevu, umepokelewa kwa mikono miwili na wazazi wa mkoa huo, walimu na hata wakuu wa idara ya elimu wakisema ni muhimu kwani pia utasaidia kuongeza maudhurio ya wanafunzi shuleni.

Mpango huo wa majaribio unaowahusisha wanafunzi takribani 10,000 wa shule za msingi 14 mkoani humo unaenda sambamba na utaratibu wa utoaji wa chakula shuleni unaotekelezwa na asilimia kubwa ya shule za mkoa huo.

Baadhi ya wazazi wamesema gharama ya Sh 2,000 ambazo wanapaswa kutoa kwa mwezi ili kufanikisha watoto wao kunywa maziwa shuleni ni jambo jema kwani itaboresha afya kuliko viburudisho vingine ambavyo watoto wao hununua kila siku wanazowapa kama matumizi.

Wamesema hawana shaka na uchangiaji wa gharama hizo hasa ikizingatiwa ni ndogo wana uwezo wa kuimudu na kusisitiza kuwa kwa kuwa shule nyingi za mkoa huo zina utaratibu wa kutoa chakula kwa wanafunzi, kuwapo kwa mpango huo wa kutoa maziwa ni jambo wanaloliunga mkono kwa asilimia 100.

Wamesema kupitia mpango huo wanafunzi kunywa maziwa mara mbili kwa wiki shuleni ni jambo linalowezekana na kueleza kuwa kama utaonesha mafanikio zaidi wapo tayari kuongeza fedha ili badala ya watoto hao kunywa maziwa mara mbili kwa wiki ziweze kuongezeka hadi kufikia tano.

Kwa mujibu wa Bodi ya Maziwa Tanzania, mpango huo umeanza kwa majaribio katika mkoa huo ba baada ya hapo utakwenda katika shule za msingi nchi nzima, pamoja na mambo mengine umelenga kuboresha afya za wanafunzi na kuwaepusha na udumavu tatizo ambalo linawakabili watoto wengi nchini.

Imesema kupitia vikao vya wazazi na kamati za shule, wamekubaliana kuwa ni vyema suala hilo walifanikishe kwa kuwa lina manufaa makubwa kwa afya za watoto lakini pia kwa ajili ya kuwaongezea uelewa darasani hivyo kuongeza ufaulu katika mitihani yao ya shule na kitaifa.

Kwa upande wao, baadhi ya walimu wakuu wa shule za msingi mkoani Arusha akiwemo wa Shule ya Msingi ya Makumbusho, Francisca Michael wamesema ujio wa mpango huo ni muhimu kwa maendeleo ya wanafunzi na shule kwa ujumla, huku wakiwataka wakuu wa shule ambao bado hawajaanza mpango huo kuchangamkia.

Ofisa Elimu Wilaya ya Longido, Pamela Materu amesema kuanzishwa kwa mpango huo ni jambo ambalo wao kama wasimamizi wa elimu wamelipokea vyema kwa kuwa lina faida kubwa kwa watoto hao na zaidi linapendeza kwa kuwa limeungwa mkono na wazazi wengi wa wilaya hiyo.

Amesema kuna umuhimu mkubwa wa utekelezaji wa mpango huo kwani utaisaidia wilaya kuendelea kupanda kitaaluma baada ya miaka ya hivi karibuni kupata matokeo mazuri katika mitihani mbalimbali kutokana na mipango mizuri iliyowekwa ikiwamo utoaji wa chakula kwa wanafunzi ambao sehemu ya gharama huchangiwa na wazazi.

**MSAMIATI WA LEO**

HabariLEO

**NUKUU**

**KITALI:**

Scanned with CamScanner

# Kizimbani wa

Na Mwandishi Wetu

WATUMISHI wanne wa Shirika la Umeme Tanzania (Tanesco), wamefikishwa katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu wakikabiliwa na mshtaka manne ikiwemo la kuongoza genge la uhalifu, wizi, kutumia nyaraka kufanya udanganyifu na kuisababishia serikali hasara ya zaidi ya Sh milioni 33.

Washtakiwa
mahakamani mw
washtakiwa hao
Ofisa manunuzi
wa Singida, Issa
ni dereva wa T
Godfrey Maleko
Tanesco Kurasi
Msoka (Ofisa
Kurasini).

Wakili wa
Martenus Mara
Wakili wa Serika

MAJIRA UK 11

# Watakiwa kufuatilia ubora wa nyama

Na oscar Mzuka, Dodoma

MAOFISA wa Halmashauri wa Jijini Dodoma, walioko kwenye sekta ya nyama, wametakiwa kufuatilia kwa ukaribu sana nyama kuanzia machinjioni na uuzaji wake ili kudhibiti nyama zenye dosarikiwemo vibudu.

Hayo yalisemwa Jijini Dodoma jana na msajili wa Baraza la Veterinari Tanzania, Dkt.Bedan Masuruli, alipokuwa akiongea na gazeti hili kuhusu ukiuwaji wa sheria za nyama, unaofanywa na baadhi ya wafanyabiashara ya nyama.

Dkt. Masuruli alisema ukiukwaji wa sheria hizo unaofanywa na baadhi ya wafanyabiashara wadau wa nyama, inachangiwa na baadhi ya maofisa wa nyama, katika kazi zao kwa kufanyakazi kwa mazoea na rushwa na hivyi kukiuka sheria ya bodi ya nyama.

"Kwa upande wetu, sisi wa Veterinari kunahakikisha sheria zetu kwa sekta ya mifugo zinafuatwa na kunafanya udhibiti wa juu, madaktari wetu wa mifungo wanazifuata, na pia kuwachukulia hatua kali ya kisheria kwa maduka ya dawa za mifugo kwa yule anapobainika kuuza dawa zilizoisha muda, na mambo mengine," alisema Dkt. Masuruli.


Aidha alisema, baraza la veterinari linafanya ukaguzi mara kwa mara kote nchini na wale waliobainika kufanya makosa yanayohusu wanyama wa mifugo, linafuata sheria na pia inaweza kuwafikisha mahakamani.

Naye ofisa mifugo wa Jijini hilo Dkt. Gratian Mwesiga,alisema kuwa alipata taarifa hizo, tunazotaka kufanyia kazi ikiwa na ile ya nyama vibudu.

Alisema kitengo chake kimeanza kufanya ukaguzi katika maeneo ya nyama Jijini Dodoma ili kudhibiti hali hiyo.

"Si rahisi kwa asilimia 100 kukabiliana nazo, tunajitahidi kuweka mambo sawa, tunashangaa kuwa nyama vibudu zinatokea wapi. Nyama tunazopima na zile za ubora tunazigonga mhuri kuzitambua," Alisema Dkt.Mwesiga.

Kwa upande mwingine ameviomba vyombo vya habari kushirikiana nao kwa ukaribu zaidi, kuibua mambo mbalimbali yanayokwenda kinyume cha Sheria ya Jiji, kwa mfano kwenye mabucha ya nyama.



Waziri Mkuu
jana katika m
Simanjiro. Pi
Mradi wa ma

# Kero

Na Mwandisi

MADIWAN
za Mzimuni na
ya Kinondoni
za watu wanne
ili kusimamia
mfereji wa Mk
unahatarisha n
hasa wakati w

Mapendekez
Kamati hizo y
mkutano wa
hizo mbili Jiji
jana ambapo
mengine ba
walilalamika ku
ambayo upele
ya nyumba zao
mnyoo kwa w

"Tunawash
kwa kuunda
tungependa m
marekebisho,
ni mbaya sa

Scanned with CamScanner

# * Serikali kutumia mil. 100/- kuimarisha Kituo Ruhila*

**Na Mbaraka Kambona, Ruvuma**

KATIBU Mkuu Wizara ya Mifugo na Uvuvi (Uvuvi), Dkt. Rashid Tamatamah amesema serikali imepanga kutumia sh. milioni 110 kwa ajili ya kuimarisha miundombinu ya Kituo cha Kutotolesha Vifaranga vya Samaki cha Ruhila, ili kiweze kuzalisha vifaranga vitakavyokidhi mahitaji yaliyopo sasa.

Dkt. Tamatamah aliyasema hayo alipotembelea na kukagua shughuli zinazofanywa na kituo hicho kilichopo mkoani Ruvuma mwishoni mwa wiki.

Alisema kwa mwaka huu wa fedha 2020/21, serikali kupitia Wizara ya Mifugo na Uvuvi imepanga kuzalisha vifaranga milioni 22 na kati ya hivyo, milioni 16 vitazalishwa na vituo vya kutotolesha vya watu binafsi na vifaranga milioni 6, vitazalishwa na vituo vya serikali.

Aliongeza kuwa hivi karibuni, Wizara itatangaza zabuni kwa ajili ya kuimarisha na kuboresha kituo hicho, ili kiweze kuwa na uwezo mkubwa zaidi wa kuzalisha vifaranga utakaowezesha kukidhi mahitaji yaliyopo sasa.

"Baada ya kukiimarisha kituo hiki mwaka huu, mwaka ujao wa fedha tutafanya ukarabati mkubwa na ukarabati huo, ukikamilika tunatarajia uwezo wa uzalishaji wa kituo hiki kuongezeka mara tatu zaidi ya sasa na hivyo kutaongeza uhakika wa upatikanaji wa vifaranga vya samaki," alisema.

Naye Mkurugenzi wa Idara ya Viumbe Maji kutoka Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Dkt. Nazael Madalla alitoa rai kwa Watanzania hasa wale wanaoishi mbali na vyanzo vikubwa vya maji kama maziwa kujihusisha na shughuli za ufugaji wa samaki kwani kwa kufanya hivyo kutawasaidia kupata kipato na lishe bora.

"Naomba Watanzania watembelee kituo hiki ili waweze kujifunza kwa vitendo namna ya kuchimba mabwawa makubwa na ufugaji samaki, ili kujiongezea kipato na lishe bora kwa ajili yao na watoto wao," alisema.

Kwa upande wake Kaimu Katibu Tawala anayeshughulikia Uchumi na Uzalishaji mkoani Ruvuma, Deogratius Sibula alisema Ruhila kimekuwa kituo muhimu kwa Mikoa ya Nyanda za Juu Kusini kwa sababu wafugaji wengi, wanategemea kituo hicho kupata vifaranga vya samaki kwa ajili ya kufuga.

"Katika Mkoa wa Ruvuma kuna wafugaji wa samaki takriban 4,000 na kuna mabwawa ya samaki zaidi ya 6,000 na wote wamekuwa wakitegemea kituo hiki kwa ajili ya kupata mbegu na kupata elimu ya ugani, hivyo ni kituo muhimu katika kuchagiza ongezeko la ufugaji wa samaki na upatikanaji wa lishe bora kwa wananchi," alisema.

Ofisa Mfawidhi wa Kituo cha Ruhila, Emmanuel Maneno alisema baadhi ya Mikoa ya Nyanda za Juu Kusini inakabiliwa na utapiamlo, hivyo fursa ya uhakika ya kuondokana na tatizo hilo ni kufuga samaki ambao watawahakikishia kupata lishe bora na kipato cha kujikimu kimaisha.

Maneno aliongeza kuwa, Mikoa ya Nyanda za Juu Kusini ina mazingira mazuri ya kufuga samaki kwa sababu hali ya hewa ni nzuri, maji yapo ya kutosha lakini pia malighafi kwa ajili ya kutengenezea chakula cha samaki, inapatikana kwa urahisi na hivyo kufanya gharama za ufugaji wa samaki kuwa chini.



Katibu Mkuu, Wizara ya Mifugo na Uvuvi (Uvuvi), Dkt. Rashid Tamatamah akinawa maji ya Ziwa Nyasa alipotembelea Kituo cha Udhibiti wa Rasilimali za Uvuvi Ziwa Nyasa kilichopo Mbamba bay wilayani Nyasa Mkoa wa Ruvuma mwishoni mwa wiki. Wa kwanza kulia ni Mkurugenzi Idara ya Ukuzaji Viumbe Maji (WMUV), Dkt. Nazael Madalla. (Picha na Mbaraka Kambona)

## Watendaji Buguruni watakiwa kujieleza kwa Meya

**Na Heri Shaaban**

MEYA wa Halmashauri ya Ilala, Omary Kumbilamoto amewataka Watendaji wa Serikali Kata ya Buguruni kujieleza kwa nini wamesusia kikao chake.

Kumbilamoto haliyasema hayo katika kikao cha Serikali ya Mtaa kilichoandaliwa na Mwenyekiti wa Mtaa huo, Bakari Uwesu kilichokuwa kikijadili maendeleo ya mtaa pamoja na ulinzi na usalama.

"Naomba Ofisa Mtendaji wa Kata ya Buguruni na timu yako, Ofisa Elimu Kata, Ofisa Afya, Ofisa Maendeleo Kata mlete maelezo kwa nini mmeshindwa kuja katika mkutano, nani ajibu kero zenu ikiwa kama nyinyi ndiyo viongozi wa kata hii," alisema.

Meya Kumbilamoto alisema katika vikao vyote ngazi ya mtaa au kata anapokwenda kiongozi

Scanned with CamScanner

TUHUMA

# Baba mbaroni akidaiwa kubaka wanawe

**Hawa Mathias**, Mwananchi
hmathias@mwananchi.co.tz

**Mbeya.** Polisi mkoani Mbeya inamshikilia Iskaka Mkumbwa (53), mkazi wa Kata ya Itende Jijini hapa kwa tuhuma za kuwabaka watoto wake wawili wa kike, huku mmoja anayesoma kidato cha tatu akipata ujauzito.

Kamanda wa polisi mkoani hapa, Urlich Matei alilieleza Mwananchi jana kuwa mtuhumiwa alitenda vitendo hivyo kwa nyakati tofauti na kuwatishia kuwaua endapo watapiga kelele.

"Kitendo kilichofanywa na mtuhumiwa sio cha kiungwana kwani baada ya mama yao kufariki, baba alikuwa akiishi na mmoja wa watoto wake anayesoma kidato cha tatu, huku mdogo wa darasa la sita alichukuliwa kulelewa na mama wa hiari ambaye ni jirani," alisema.

Alieleza mtuhumiwa alikamatwa na watoto hao walitoa ushirikiano wa kueleza namna baba yao alivyokuwa akiwafanyia vitendo hivyokwa nyakati tofauti. Alisema mtuhumiwa atafikishwa mahakamani baada ya uchunguzi, huku akiwataka wananchi kuwafichua wazazi wenye tabia za aina hiyo.

Dada wa watoto hao alidai alibaini wadogo zake kuingiliwa kimwili na baba yao baada ya mmoja wao kupimwa na kukutwa ana ujauzito wa miezi mitatu na alipohojiwa, alimtaja baba yao kuhusika. "Mdogo wake alikiri kuwa baba yao amekuwa akimwita chumbani na kumbaka, huku akimtishia kuwa akipiga kelele atamuua," alisema.

**TAARIFA ZAIDI**

Mwenyekiti wa Mtaa, Obed Mahema alieleza baada ya kupata taarifa hizo alitoa taarifa kwa viongozi wa kata akiwepo diwani na mtuhumiwa kukamatwa.

Aliomba Serikali kuivalia njuga suala hilo, kwani kata hiyo kesi nyingi za ukabaji na mimba za utotoni zimekuwa zikilishia ngazi za familia.

MWANANCHI UK 24



**ZIARA**

Katibu Mkuu Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Dk Rashid Tamatamah akinawa katika Ziwa Nyasa alipotembelea Kituo cha Udhibiti wa Rasilimali za Uvuvi Ziwa Nyasa kilichopo Mbamba Bay, wilayani Nyasa, mkoani Ruvuma, juzi. Kulia ni Mkurugenzi, Idara ya Ukuzaji Viumbe Maji (WMUV), Dk Nazael Madalla. Picha na WMUV

Scanned with CamScanner

# Kanuni za uvuvi kupitiwa upya

**Na Mbaraka Kambona, Dodoma**

■■Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Mashimba Ndaki amesema kufuatia changamoto zilizojitokeza katika utekelezaji wa marekebisho ya kanuni za uvuvi za mwaka 2020 serikali imeazimia kuzipitia upya ili ziendane na mahitaji ya sasa.

Ndaki aliyasema hayo juzi jijini Dodoma wakati akiongea na Waandishi wa Habari na kutoa ufafanuzi kuhusu matumizi ya zana za uvuvi katika maji yote nchini.

Alisema hivi karibuni Wizara imepokea maoni na changamoto mbalimbali kutoka kwa wadau wa sekta ya uvuvi kutoka Ukanda wa Bahari, Ziwa Tanganyika, Ziwa Victoria kuhusiana na marekebisho ya kanuni ya uvuvi ya mwaka 2020 katika baadhi ya vipengele.

Ndaki alisema kuwa maeneo ambayo yameonesha kuwa na changamoto nyingi ni katika uvuvi wa kutumia nyavu za mtando (Ring net) wakati wa mchana katika ukanda wa Bahari ya Hindi, utaratibu wa kupima ukubwa wa macho ya nyavu kwa kutumia kipimo kilichoainishwa katika kanuni kinachofahamika kama Mesh Gauge na uvuvi wa Dagaa wakati wa mbalamwezi.

Kufuatia changamoto hizo, Waziri Ndaki alitoa maelekezo kuwa Taasisi ya Utafiti wa Uvuvi Tanzania (TAFIRI) ifanye utafiti kuhusu uvuvi wa kutumia nyavu za mtando na iwasilishe taarifa kwa Waziri huyo ndani ya siku kumi na nne (14) ili serikali iweze kutoa maelekezo .

Kuhusu utaratibu wa kipimo cha ukubwa wa nyavu, Waziri alisema kuwa watashirikiana na Shirika la Viwango Tanzania (TBS) na watatoa maelekezo ni kipimo gani kitumike lakini kwa sasa utaratibu wa kupima nyavu uendelee kama ilivyokuwa awali kwa kutumia kipimo cha Venier Calliper.

Pia, Ndaki aliwaagiza wataalamu wa wizara kutoa haraka mwongozo kuhusu uvuvi wa Dagaa wakati wa mbalamwezi ili kuondoa sintofahamu iliyopo sasa ya wakati gani hasa uvuvi huo ufanyike.

Aidha, Ndaki aliongeza kwa kusema kuwa wizara yake itapitia upya marekebisho ya kanuni zote za uvuvi na kuharakisha marekebisho ya kanuni nzima ya Mwaka 2009 ili iendane na wakati.

Katika hatua nyingine, Ndaki alitoa wito kwa wadau wa sekta ya uvuvi wakiwemo wavuvi na wafanyabiashara kuendelea kutoa ushirikiano kwa serikali ili kuhakikisha shughuli za uvuvi zinaendeshwa kwa ushirikishwaji na kunakuwa na uvuvi endelevu wenye tija.

Ndaki aliziagiza Halmashauri zote nchini kushirikiana na jamii za wavuvi kusimamia kikamilifu rasilimali za uvuvi kwa mujibu wa sheria zilizopo huku akiwakumbusha wafanyabiashara wa zana za uvuvi na viwanda vya kutengeneza zana za uvuvi kuzalisha na kuuza zana zinazokubalika kisheria.



Katibu Tawala wa Wilaya ya Uyui Moses Pesha akitoa salamu za Serikali jana wakati wa kikao cha Baraza la Madiwani ambalo lilipitisha mapendekezo ya makisio ya shilingi bilioni 34.2 kwa ajili ya mapato na matumizi ya mwaka ujao wa fedha. (Picha na Vincent Tiganya)

unguza
mavu

Morogoro

wa hali ya
walio chini
i Morogoro
toka asilimia
3,4 mwaka
rikali kutoa
tia masuala
wa watoto
wazito na
zaa.
ana mkoani
mkoa wa
Magembe,
athmini ya
elezaji wa
ja na Bima
CHF).
wa hali ya
ilo mkoani
a mwaka
na elimu
wahudumu
nbapo kila
afya wawili
wa kutoa
a na jamii

kushuka
Morogoro
a mkataba
aka 2018
mikoa na
muhuri ya
kwa niaba

u wa mkoa
le Sanare
aliwataka
nauri zote
lingi 1000
a chini ya
a mapato
esha lishe

elfu moja
elekezwa
i kutoka
a mapato
boresha
e umri wa
natolewa
fu kama
anare.
i vyema
a huo
a katika
ya iCHF
wezesha
u wakati
uma hiyo.
Morogoro
na kuwa
ekwisha
wa bima

Scanned with CamScanner

...ONI 110/- >> Kuimarisha miundombinu ya kituo cha kutotolesha vifaranga vya samaki

# Kituo cha kutotolesha vifaranga kuimarishwa

**Na MWANDISHI WETU,** *Ruvuma*

WIZARA ya Mifugo na Uvuvi, imepanga kutumia sh. milioni 110 kuimarisha miundombinu ya Kituo cha Kutotolesha vifaranga vya samaki cha Ruhila, ili kizalishe vifaranga vitakavyokidhi mahitaji yaliyopo sasa.

Kauli hiyo ilitolewa mwishoni mwa wiki iliyopita na Katibu Mkuu wa wizara hiyo anayeshughulikia uvuvi, Dk. Rashid Tamatamah, alipokagua shughuli zinazofanywa na kituo hicho kilichopo Mkoani Ruvuma.

Alisema kwa mwaka huu wa fedha 2020/2021, serikali kupitia wizara hiyo ilipanga kuzalisha vifaranga milioni 22 na kati ya hivyo milioni 16 vitazalishwa na vituo vya kutotolesha vya watu binafsi na milioni sita vitazalishwa na vituo vya serikali.

Dk. Tamatamah alisema hivi karibu watatangaza zabuni kwa ajili ya kuimarisha na kuboresha kituo hicho ili kiwe na uwezo mkubwa zaidi wa kuzalisha vifaranga utakaokidhi mahitaji yaliyopo sasa.

"Baada ya kukiimarisha kituo hiki mwaka huu, mwaka ujao wa fedha tutafanya ukarabati mkubwa ambao ukikamilika tunatarajia uwezo wa uzalishaji utaongezeka mara tatu zaidi ya sasa, hivyo kutakuwa na uhakika wa upatikanaji wa vifaranga vya samaki,"alisema.

Mkurugenzi wa Idara ya Viumbe Maji kutoka Wizara hiyo, Dk. Nazael Madalla, alitoa rai kwa Watanzania hususan wanaoishi mbali na vyanzo vikubwa vya maji kama maziwa kujihusisha na shughuli za ufugaji wa samaki, kwa kuwa kutawasaidia kupata kipato na lishe bora.

"Naomba Watanzania watembelee kituo hiki wajifunze kwa vitendo namna ya kuchimba mabwawa makubwa na kufugaji samaki ili kujiongezea kipato na lishe bora kwa ajili yao na watoto wao," alisema.

Kaimu Katibu Tawala anayeshughulikia Uchumi na Uzalishaji Mkoani hapa, Deogratius Sibula, alisema Ruhila kimekuwa kituo muhimu kwa mikoa ya nyanda za juu kusini kwa sababu wafugaji wengi wanategemea kituo hicho kupata vifaranga vya samaki kwa ajili ya kufuga.

"Katika Mkoa wa Ruvuma kuna wafugaji wa samaki takriban 4,000 huku kukiwa na mabwawa ya samaki zaidi ya 6,000 na wote wamekuwa wakitegemea kituo hiki kwa ajili ya kupata mbegu na kupata elimu ya ugani.

Hivyo, hiki ni kituo muhimu sana katika kuchagiza ongezeko la ufugaji wa samaki na upatikanaji wa lishe bora kwa wananchi," alisema.

Ofisa Mfawidhi wa Kituo cha Ruhila, Emmanuel Maneno, alisema baadhi ya mikoa ya nyanda za juu kusini inakabiliwa na utapiamlo, hivyo fursa ya uhakika ya kuondokana na tatizo hilo ni kufuga samaki ambao watawahakikishia kupata lishe bora na kipato cha kujikimu kimaisha.

Maneno alisema mikoa hiyo ina mazingira mazuri ya kufuga samaki kwa sababu hali ya hewa ni nzuri, maji yapo ya kutosha, pia malighafi kwa ajili ya kutengenezea chakula cha samaki inapatikana kwa urahisi, hivyo kufanya gharama za ufugaji wa samaki kuwa chini.

**VIFARANGA**



KATIBU Mkuu wa Wizara ya Mifugo na Uvuvi (Uvuvi), Dk. Rashid Tamatamah (katikati), akipata maelezo kutoka kwa Ofisa Mfawidhi wa Kituo cha Kutotolesha Vifaranga vya Samaki Ruhila, Emmanuel Maneno, kuhusu kituo hicho, Mbamba Bay, Wilaya ya Nyasa mkoani Ruvuma, mwishoni mwa wiki. Kulia ni Mkurugenzi wa Ukuzaji Viumbe Maji katika wizara hiyo, Dk. Nazael Madalla.

## Wananchi Ruangwa wavutiwa utekelezaji wa Ilani ya CCM

**NA SOPHIA NYALUSI,** *Ruangwa*

WANANCHI wa Wilaya ya Ruangwa, Mkoani Lindi, wameeleza kuvutiwa na Chama cha Mapinduzi (CCM), jinsi kinavyofanya kazi zake katika kuhakikisha Ilani ya Uchaguzi ya Chama inavyotekelezwa maeneo mbalimbali.

Kauli hiyo ilitolewa mwishoni mwa wiki iliyopita na baadhi ya wakazi wa Wilaya hiyo akiwemo Jane Mdemu, wakati wa maadhimisho ya miaka 44 ya kuzaliwa kwa CCM ambayo katika mkoa wa Lindi, yalifanyika Wilaya ya Ruangwa.

Jane alisema CCM imefanya kazi nzuri katika sekta mbalimbali hususan afya, umeme na elimu ambapo kila kata kuna shule za sekondari.

"Kila kijiji kina umeme na zahanati yake, hivyo tunampongeza Rais Dk. John Magufuli na Mbunge wa Ruangwa, Kassim Majaliwa (Waziri Mkuu), kwa kuleta maendeleo makubwa katika Wilaya yetu," alisema.

Aliongeza kuwa: "Katika Wilaya yetu ya Ruangwa, kuna shule ya sekondari ya wasichana Lukasi Maria, ambayo kwa sasa inapokea hadi kidato cha tano na sita, hizo zote ni juhudi ya serikali ya awamu ya tano chini ya Rais Dk. Magufuli kwa kuona Wilaya ya Ruangwa nayo inakuwa na ufaulu mzuri wa wanafunzi."

Peter Muhongolo alisema Mbunge wa Jimbo la Ruangwa, Majaliwa ameliletea jimbo hilo maendeleo yakiwemo kila kijiji kuna umeme, maji na kuhakikisha barabara za kila eneo zinapitika.

"Wananchi wa Ruangwa tunamuombea kila lenye kheri katika kuhakikisha anakuwa na afya nzuri ili ashughulikie matatizo yote ambayo kwa asilimia 98 ameyatatua katika kila sekta,"alisema.

Mwenezi wa CCM Mkoa Lindi, Amiri Mkalipa, alisema serikali imefanya kazi kubwa katika Wilaya Ruangwa kuhakikisha inawaletea maendeleo wananchi wake.

Alisema mbunge wa Jimbo hilo, ameendelea kuleta wawekezaji ili kuitanua Wilaya ya Ruangwa na kuwa na ajira nyingi kwa vijana kutokana na ujenzi wa viwanda, hivyo waliwaomba wananchi waendelee kuiamini CCM katika kuwatumikia.

**UTEKELEZAJI ILANI**

**MAENDELEO**

Kila kijiji kina umeme na zahanati yake, hivyo tunampongeza Rais Dk. John Magufuli na Mbunge wa Ruangwa, Kassim Majaliwa (Waziri Mkuu), kwa kuleta maendeleo makubwa katika Wilaya yetu.

Scanned with CamScanner

## HABARI KITAIFA

NIPASHE UK 10.

# Mbaroni tuhuma kutorosha mifugo mipakani

**Na Mwandishi Wetu,** TANGA

JESHI la Polisi Mkoa wa Tanga kwa kushirikiana na Wizara ya Mifugo na Uvuvi limewakamata watuhumiwa wawili wa utoroshaji wa mifugo maeneo ya mipakani.

Kwa mujibu wa Kamanda wa Polisi Mkoa wa Tanga, Blasius Chatanda, watuhumiwa hao wamekamatwa kufuatia operesheni kubwa iliyoanzishwa hivi karibuni, ambayo lengo lake ni kudhibiti matukio ya wizi wa mifugo pamoja na usafirishaji wake nje ya nchi bila kufuata utaratibu.

Kamanda Chatanda alisema pamoja na kuwakamata watuhumiwa hao wawili, Jeshi hilo linaendelea kuwatafuta wengine ambao wamekuwa wakijishughulisha na utoroshaji huo wa mifugo kinyume cha taratibu.

"Mpaka wetu wa Horohoro ni miongoni mwa mipaka inayoweza kutumika kupeleka mifugo nje ya nchi hususani nchi jirani ya Kenya na pia bahari yetu ya Hindi nayo inaweza kutumiwa kuvusha mifugo kupeleka Tanzania Visiwani, Comoro, Ushelisheli na Madagascar," alisema Chatanda.

"Ndio maana tukaanzisha operesheni hii kabambe, na katika eneo hili la Wilaya ya Mkinga kulikuwa na watuhumiwa watatu ambao walikuwa wakidaiwa kusumbua sana katika eneo hili, tumewakamata wawili ambao wameunganishwa na wengine waliokamatwa Arusha na taratibu za uchunguzi zinaendelea ili hatimaye wafikishwe mahakamani."

Alisema mkoa wa Tanga ni kati ya mikoa yenye wafugaji wengi na kuwataka wale wote wanaojihusisha na vitendo vya utoroshaji wa mifugo waache mara moja na kwamba mkono wa sheria hautawaacha salama endapo wataendelea na vitendo hivyo.

"Katika mpaka wa Horohoro kwa miaka mingi mifugo ilikuwa inavushwa bila kufuata utaratibu, kwa sababu ilikuwa inapitishwa katika njia zisizo rasmi na kwenda kwenye soko la nchi jirani hali ambayo ilichangia wafugaji kuuza mifugo kwa hasara na wengine kupoteza mifugo wakati wa kuvuka kwenda huko," alisema Chatanda.

"Na baada ya kufanya uchunguzi tulibaini kwamba wapokeaji wengi wa mifugo hiyo walikuwa mpakani na wengine walikuwa na madaraka kwenye maeneo wanayoishi, hivyo endapo suala hili lingeendelea kuachwa lingesabisha hasara kubwa. Serikali ina mkono mrefu tumejipanga vizuri kukomesha vitendo hivi na tunawataka wale wote iokuwa wanafanya hivyo waache mara moja kwa maana hawako salama."

Wiki iliyopota, Waziri wa Mifugo na Uvuvi Mashimba Ndaki aliagiza kukamatwa kwa watu wanaojihusisha na utoroshaji wa mifugo kwenda nchi za nje.

## Exim Benki: Tumepata faida licha ya Covid-19

**Na Mwandishi Wetu**

BENKI ya Exim (Group) imetangaza kupata faida ya jumla ya Sh. bilioni 25.3 (kabla ya kodi) kwa mwaka 2020 ikilinganishwa na hasara ya kiasi cha Sh. bilioni 8.4 bilioni iliyopata kwa mwaka uliopita, hatua inayoakisi ukuaji wa asilimia 402 wa mwaka hadi mwaka.

Mafanikio hayo vanay-

Scanned with CamScanner